



JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA

OFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOZA NA SERIKALI ZA MITAA



HALMASHAURI YA MANISPAA YA SHINYANGA

Ofisi ya Mkuu rgenzi wa Manispaa, S.L.P. 28, Chamaguha, Shinyanga.

Simu: 028-2763213, Baruaapepe: md@shinyangamc.go.tz, tovuti: www.shinyangamc.go.tz

10/05/2021

TANGAZO LA ZABUNI

Halmashauri ya Manispaa ya Shinyanga inakaribisha maombi ya Zabuni toka kwa Makampuni yenye sifa stahiki na uwezo kisheria kufanya kazi ya huduma ya uwakala wa ukusanyaji mapato kama inavyojionyesha katika jedwali hapa chini, kwa mwaka wa fedha 2021-2022, kuanzia tarehe 01/07/2021 hadi tarehe 30/06/2022.

NAMBA YA ZABUNI	AINA YA ZABUNI	IDADI YA "LOT"	ADA YA ZABUNI
LGA/112/2021-2022/HQ/REV/01	<p>Uwakala wa kukusanya mapato vyoo vya Umma,</p> <ul style="list-style-type: none">• Choo cha Ibinzamata• Choo-soko la Ndala• Choo-soko kuu• Choo -Stendi ya wilaya (banda la wasafiri)• Choo kipyä stendi ya wilaya.• Choo-soko nguzo nane• Choo-Ngokolo mitumbani• Choo- Kambarage• Choo-Lubaga• Choo-soko la Chamaguha• Choo cha wamachinga	11	50,000/=

LGA/112/2021-2022/HQ/REV/02	<p>Uwakala wa kukusanya mapato kwenye minyororo ya Stendi .</p> <ul style="list-style-type: none"> • Stendi kuu ya Ibinzamata • Stendi ya wilaya • Stendi ya soko kuu 	3	50,000/=
LGA/112/2021-2022/HQ/REV/03	<p>Uwakala wa kukusanya ushuru kwenye mnada wa Old Shinyanga,machinjio ya Old Shinyanga na mapakilio.</p>	1	50,000/=
LGA/112/2021-2022/HQ/REV/04	Ushuru wa mazao	1	50,000/=
LGA/112/2021-2022/HQ/REV/05	<p>Matangazo ya Stendi.</p> <ul style="list-style-type: none"> • Stendi kuu ya Mkoa Ibinzamata • Stendi ya wilaya 	2	50,000/=
LGA/112/2021-2022/HQ/REV/06	<ul style="list-style-type: none"> • Machinjio ya nguruwe Karogho 	1	50,0000/=
LGA/112/2021-2022/HQ/REV/07	Ushuru wa madini Ujenzi	1	50,000/=

1. BARUA ZA MAOMBI ZIAMBATANISHWE NA MAELEZO KAMILI NA VIVULI VILIVYOTHIBITISHWA KAMA IFUATAVYO:-

1. Leseni (halali) ya Biashara husika.
2. Hati ya kuandikishwa kwa Kampuni
3. Stakabadhi uliyolipia Ada ya Maombi ya Zabuni
4. Maelezo ya kazi ulizowahi kufanya na uzoefu usiopungua miaka miwili wa huduma ya Uwakala wa ukusanyaji Mapato na Vielelezo vilivyothibitishwa na Waajiri wa awali kwa kazi husika.
5. Usajili wa TIN

6. Muombaji ataje kiasi (Asilimia ya Commission atakayolipwa) na Halmashauri kutokana na mchanganuo wake kati ya asilimia 1% -20%.
7. Muombaji aonyeshe idadi ya Wafanyakazi/Watendaji wake pamoja na sifa za Kitaalumu, Uzoefu/Ujuzi na Maadili ya kazi ya Huduma ya Ukusanyaji Mapato [uthibitisho unahitajika].
8. Uthibitisho wa uwezo wa Muombaji kifedha kwa kuonyesha Taarifa ya Fedha ya Benki (Bank Statement) ya miezi mitatu ya hivi karibuni iliyoidhinishwa na kuthibitishwa na Meneja wa Tawi la Benki husika.
9. Muombaji aambatanishe uhalali wa kisheria (Power of Attorney) ya mtu atakayehusika na Zabuni hii.
10. Taarifa ya madeni yake yote [kama yapo] anayodaiwa na watu binafsi, Benki au Taasisi nyingine.
11. Mzabuni anaweza kuomba zaidi ya Chanzo kimoja, Kila aina ya zabuni italipiwa ada kama ilivyoonyeshwa katika jedwali.
 - (i) Zabuni itakayowasilishwa bila kukamilika itaondolewa katika hatua za awali.
 - (ii) Tathimini na tuzo itatolewa kwa Mzabuni kwa kuzingatia chanzo kimoja alichoshinda au mchanganyiko wa Vyano.
12. Zabuni hii ni maalumu kwa wakazi wa Mkoa wa Shinyanga (**PPA 2011 Sec 40**)
 15. Mwisho wa kurudisha maombi ya zabuni ni tarehe **25/05/2021**saa **4.00** asubuhi siku ya Jumanne ambayo ufunguzi utafanyika.. Juu ya bahasha yaandikwe maandishi yanayotaja aina ya zabuni unayoomba,Zabuni hizo zipelekwe katika sanduku la zabuni lilipo ofisi ya manunuizi,kwa kutumia anuani ifuatayo:-
Mkurugenzi wa Manispaa, Manispaa ya Shinyanga, S.L.P. 28, SHINYANGA. Zabuni itakayochelewa haitafunguliwa. Kabrasha la Zabuni lina patikana Ofisi ya manunuizi kwa Katibu wa Bodi ya Zabuni. Mwombaji/Mwakilishi anaruhusiwa kuhudhuria ufunguzi wa zabuni utakaofanyika tarehe 25/05/2021 saa 4.00 asubuhi, kwenye Ukumbi wa Manispaa ya Shinyanga.



Geoffrey.R.Mwangulumbi

MKURUGENZI MANISPAA

SHINYANGA

**MKURUGENZI VIA MANISPAA
HALMASHAURI YA MANISPAA
SHINYANGA**